



UNIVERSITY OF IRINGA (UoI)

CHUO KIKUU CHA IRINGA

PUBLIC RELATIONS OFFICE

(Formerly, Tumaini University, Iringa University College)

P. O. Box 200 Iringa, Tanzania, East Africa Tel: (0) 26 272-0900 Fax: (0) 26 272-0904 E-mail: uoi@uoi.ac.tz
Website: www.uoi.ac.tz

TAARIFA KWA UMMA JUU YA KUREJEA KWA MUHULA WA PILI WA MASOMO KWA MWAKA 2019/2020

Uongozi wa Chuo Kikuu cha Iringa, unapenda kuwatangazia wafanyakazi wake, wanafunzi, na umma kwa ujumla kuwa, kutokana na taarifa iliyotolewa na Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. John Pombe Magufuli tarehe 21/05/2020 na kuvitaka Vyuo Vikuu vyote nchini kurejea katika shughuli zake za kawaida na kuendelea na masomo.

Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe 01/06/2020 kama ilivyo tangazwa. Uongozi wa Chuo unawasisitiza wanafunzi wote kuwa wanatakiwa kuwepo Chuoni na kuanza masomo tarehe hiyo, na pia kufuata taratibu zote za Chuo ikiwemo kulipa ada kwa wakati na kuzingatia ratiba ya masomo.

Wakati huo huo, Uongozi wa Chuo Kikuu cha Iringa unaendelea kuchukua tahadhari juu maambukizi ya virusi vya COVID-19, na kuwaomba Wafanyakazi, wanafunzi, na wageni wote waingiapo Chuoni wanawe mikono sehemu zilizoandaliwa na Chuo, na pia wawe wamevaa barakoa, na kuwa na vitakasa mikono (Sanitizer) watakavyokuwa wanavitumia mara kwa mara ili kukomesha kabisa kuenea kwa ugonjwa huo. Vile vile kuendela kufuata kanuni za afya na utaratibu wote unaotolewa na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto pamoja na wataalamu wa afya.

Uongozi wa Chuo Kikuu cha Iringa unaipongeza Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Raisi wake Mh. John Pombe Magufuli kupitia Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto kwa jinsi wanavyochukua hatua za kudhibiti maambukizi ya virusi vya COVID-19, kuondoa hofu na kuendeleza shughuli za kiuchumi kwa Watanzania.


Crispin Nyomoye



Afisa Mahusiano, Chuo Kikuu cha Iringa

0654 053511/ 0752 665879

26 May, 2020.